(١)

رمضان شهر الإيمان وصناعة الرجال

**Ramadhai ni mwezi wa imani na kuwajenga wanaume**

Hotuba yetu ya Ijumaa kwa anwani ya رمضان شهر الإيمان وصناعة الرجال **Ramadhai ni mwezi wa imani na kuwajenga wanaume)**kutoka wizara ya waqfu ya Misri,na Mimi ni profesa Ayman Alasar.

Hotuba ya kwanza tunazungumzia **fadhila ya Imani** na ya pili tunazungumzia **mwezi wa ramadhani ni mwezi wa kuwajenga wanaume.**

Sifa zote njema ni zake mwenyezi Mungu Mtukufu Mola wa viumbe vyote, anayesema katika Kitabu chake Kitakatifu:

بسم الله الرحمن الرحيم.

**{مِنَ الْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ عَلَيْهِ فَمِنْهُم مَّن قَضَى نَحْبَهُ وَمِنْهُم مَّن يَنتَظِرُ وَمَا بَدَّلُوا تَبْدِيلًا}**

{Miongoni mwa Waumini wapo watu walio timiza waliyo ahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwisha kufa, na baadhi wanangojea, wala hawakubadilisha (ahadi) hata kidogo}.

Na ninashuhudia kuwa hakuna Mungu mwingine aabudiwaye kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, peke yake hana mshirika wake. Na ninashuhudia kuwa Bwana wetu na Mtume wetu Muhammad ni Mja na Mjumbe wake. Ewe Mola wangu, mpe salamu na baraka Mtume wetu, na Watu wake na kila mwenye kuwafuata kwa Wema mpaka siku ya Malipo.

Na baada ya Utangulizi huu,

Hakika Kumwamini Mwenyezi Mungu Mtukufu ni katika nea Bora zaidi alizowaneemesha Waja wake. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

بسم الله الرحمن الرحيم.

**{.. وَلَكِنَّ اللَّهَ حَبَّبَ إِلَيْكُمُ الْإِيمَانَ وَزَيَّنَهُ فِي قُلُوبِكُمْ وَكَرَّهَ إِلَيْكُمُ الْكُفْرَ وَالْفُسُوقَ وَالْعِصْيَانَ أُولَئِكَ هُمُ الرَّاشِدُونَ * فَضْلًا مِنَ اللَّهِ وَنِعْمَةً وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ}.**

**{Lakini Mwenyezi Mungu amekupendezeeni Imani, na akaipamba katika nyoyo zenu, na amekufanyeni muuchukie ukafiri, na upotovu, na uasi. Hao ndio walio ongoka Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu na neema zake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye hikima}.**

Na hapana shaka kwamba Mwezi wa Ramadhani uliobarikiwa ni Mwezi wa Imani ya Kweli na kwa hivyo, aya za Mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani katika Qurani Tukufu, zimeanza kwa wito wa kiimani. Ni kama katika kauli yake yafuatayo:

بسم الله الرحمن الرحيم.

**{يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ}.**

{Enyi mlio amini! Mmeandikiwa Saumu, kama waliyo andikiwa walio kuwa kabla yenu ili mpate kuchamngu}.

Na imani ya kweli ni kukiamini kila kilicholetwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kukifanyia kazi kama kilivyo. Na imekuja katika Hadithi ya Jiburilu A.S, ambayo ni mashuhuri yenye ufafanuzi wa Ukweli wa Imani ambayo inapaswa kujengeka ndani ya Moyo wa muumini, pale Jiburilu

alipomuuliza Mtume S.A.W Kuhusu imani: Mtume (S.A.W) akasema:

**الايمان (أَنْ تُؤْمِنَ بِاللَّهِ ، وَمَلَائِكَتِهِ ، وَكُتُبِهِ ، وَرُسُلِهِ ، وَالْيَوْمِ الْآخِرِ، وَتُؤْمِنَ بِالْقَدَرِ خَيْرِهِ وَشَرِّهِ)**

Imani Ni kumuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu, na Malaika wake, na Vitabu vyake, na Mitume wake, na Siku ya Mwisho, na kuamini Kadari, Shari yake na Kheri yake.

Kwa hiyo Imani sio maneno yasemwayo mdomoni tu, lakini Imani ni kile kilichotulia moyoni na kikathibitishwa na vitendo.

**وفي ذلك يقول سبحانه تعالى عن المؤمنين :بسم الله الرحمن الرحيم**

**: {إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَتْ قُلُوبُهُمْ وَإِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ آيَاتُهُ زَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَعَلَى رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ *الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنْفِقُونَ * أُولَئِكَ هُمُ الْمُؤْمِنُونَ حَقًّا}.**

**Yaani Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema {Hakika Waumini ni wale ambao anapo tajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hujaa khofu, na wanapo somewa Aya zake huwazidisha Imani, na wakamtegemea Mola wao Mlezi. . Hao ambao wanashika Sala na wanatoa katika yale tunayo waruzuku. Hao kweli ndio Wauumini}.**

**، ويقول (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) : (الْمُسْلِمُ مَنْ سَلِمَ الْمُسْلِمُونَ مِنْ لِسَانِهِ وَيَدِهِ، وَالْمُؤْمِنُ مِنْ أَمِنَهُ النَّاسُ عَلَى أَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ ).**

**Na Mtume S.A.W anasema: Muislamu ni yule ambaye Waislamu wenzake wamesalimika kutokana na ulimi wake na mikono yake, na Muumini ni yule ambaye Watu wamemuamini kwa Mali na Nafsi zao.**

Ama kwa yule atakaye kengeuka kitabia na kivitendo akaacha maamrisho yake Mwenyezi Mungu Mtukufu na Makatazo yake basi atakuwa ametoka katika njia ya Imani ya kweli. Na katika hilo, Mtume S.A.W anasema: Mzinifu hazini wakati anazini

akawa Muumini, na wala hanywi mtu pombe Wakati anainywa akawa Muumini, na wala haibi mtu wakati anaiba akawa Muumini.

Na Mtume S.A.W ameweka wazi kwamba Imani haikamiliki kwa yule mwenye kumuudhi jirani yake, au yule aliyelala na shibe wakati jirani yake ana njaa na yeye anajua hivyo. Kwani Imani ya kweli hapana budi iambatane na vitendo. Na hapo ndipo Mtume S.A.W aliposema: Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, haamini, Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu haamini, ninaapa kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, haamini. Akaulizwa Mtume S.A.W, ni nani huyo ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu? Akasema: Ni yule mtu ambaye Jirani yake hasalimiki na Shari zake za aina zote. Na anasema Mtume S.A.W: Atakuwa hajaniamini yule atakaye lala ameshiba na jirani yake ana njaa pembezoni mwake na yeye anajua hivyo.

Kwa hiyo Imani ya kweli ni ile inayomlinda mwenye kuwa nayo kutokana na kukiuka haki za wengine, na kuwashambulia. Na imani ya kweli hukisafisha kifua cha mwenye kuwa nayo kwa kutoa gubu na husda, umimi na kujivuna, chuki, dharau na hiana, ufisadi na uharibifu. Na imani ya kweli humfundisha mtu Tabia njema, na athari yake ikadhihiri katika mwenendo wake na katika kila anachokifanya Duniani na katika Maisha yake, na jinsi anavyotangamana na viumbe vyote vya Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kuwahurumia Watu na wanyama, na hata visivyokuwa na uhai kama vile mawe na kadhalika. Akayafanya yote hayo kwa kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu.Na jambo hilo ni wazi sana katika kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu yafuatayo:

بسم الله الرحمن الرحيم.

**{وَيُطْعِمُونَ الطَّعَامَ عَلَى حُبِّهِ مِسْكِينًا وَيَتِيمًا وَأَسِيرًا * إِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ اللَّهِ لَا نُرِيدُ مِنْكُمْ جَزَاءً وَلَا شُكُورًا}.**

{Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa.Hakika sisi tunakulisheni kwa wajihi wa Mwenyezi Mungu. Hatutaki kwenu malipo wala shukrani}.

Na Imani ni Mti wenye asili isiyotetereka. Tawi lake liko mbinguni, na asili zake zinapokuwa na nguvu na mizizi yake ikaimarika basi huleta Matunda yake kila wakati kwa idhini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na Swaumu ya kweli hutokana na Imani ya aina hii, na ikaingiza Utulivu katika Nafsi ya mja na pia kumwogopa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Unamuona mwenye Swaumu ya kweli hadanganyi, kwa sababu Swaumu na uongo au udanganyifu havikutani kabisa. Swaumu inasimamia viwango vya juu vya kumwogopa Mwenyezi Mungu Mtukufu katika siri kabla ya uwazi. Na Swaumu ni siri ya mja na Mola wake, na Uongo ni katika alama za wazi za Unafiki na ni ya juu katika ngazi za Unafiki huo. Huku ni kukinzana kwa kiasi kikubwa na ukweli wa Swaumu. Na kwa hivyo, Uongo na Swaumu kamwe haviwezi kukutana. Mtu anapaswa kuchagua afunge au awe muongo. Na kwa ajili hiyo, anasema Mtume wetu S.A.W: Mtu yoyote asiyeacha maneno ya uongo na kuyafanyia kazi, basi hana haja ya kukiacha chakula chake na kinywaji chake.

Na Mtume S.A.W alipoulizwa: Je Muumini anaweza akawa mwoga? Akasema S.A.W: Ndio. Akaulizwa: Je Muumini anaweza akawa bahili? Akasema: Ndio. Akaulizwa. Je Muumini anaweza akawa mwongo? Mtume S.A.W akasema: Hapana.

Sisi sote tunaamini kuwa Imani ya kweli ni nuru inayowekwa katika Moyo wa Mja na Mwenyezi Mungu Mtukufu, na humrithisha Hekima na Yakini na humjaalia akawa anaona kwa Nuru ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na kutoka kwa Anas bin Malik, R.A anasema:  kwamba Mtume S.A.W, alitoka siku moja akakutana na kijana mmoja miongoni mwa Answari (Maswahaba wa Madina), anaeitwa: Harithah bin Nuuman, akamwambia: Umeamkaje ewe Harithah? Akasema: Nimeamka nikiwa Muumini wa kweli. Anasema: Akasema Mtume S.A.W: Yaangalie uyasemayo. Kwani kila Haki ina ukweli wake, ni upi ukweli wa Imani yako? Akasema: Nimeitenga Nafsi yangu na Dunia, na nikaukesha usiku wangu, nikaufunga mchana wangu, nikawa kama ninaiangalia Arshi ya Mola wangu huku ikiwa imejitokeza, kama vile mimi ninawaangalia Watu wa Peponi jinsi wanavyotembeleana ndani ya Pepo hiyo, na ni kama vile Mimi ninawaangalia Watu wa Motoni jinsi wanavyopishana ndani yake. Mtume S.A.W akamwambia: Umeona na uendelee kufanya hivyo. (Akasema maneno haya mara mbili). Mwenyezi Mungu Mtukufu ameutia nuru ya Imani moyo wake.

Na Imani ina sehemu nyingi ambazo kila muumini anapaswa kuzifuata. Anasema Mtume S.A.W: Imani ina sehemu sabini na kitu, na kauli iliyo bora katika hizo ni

kusema "Hakuna Mungu mwingine anaestahiki kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na jambo dogo kabisa ni kuondosha maudhi njiani. Na Haya ni sehemu ya Imani.

Na Mtu mmoja alipomuuliza Hasani Basriy R.A: Je wewe ni Muumini? Akamwambia: Imani ziko za aina mbili. Na ikiwa unaniuliza kuhusi Kumwamini Mwenyezi Mungu Mtukufu na Malaika wake, Pepo, Moto, Kufufuliwa na Kuhesabiwa, basi hakika mimi ninayaamini yote hayo. Na ikiwa unaniuliza kuhusi kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ifuatayo:

بسم الله الرحمن الرحيم.

**{إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَتْ قُلُوبُهُمْ وَإِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ آيَاتُهُ زَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَعَلَى رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ * الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنْفِقُونَ * أُولَئِكَ هُمُ الْمُؤْمِنُونَ حَقًّا}.**

{Hakika Waumini ni wale ambao anapo tajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hujaa khofu, na wanapo somewa Aya zake huwazidisha Imani, na wakamtegemea Mola wao Mlezi. Hao ambao wanashika Sala na wanatoa katika yale tunayo waruzuku. Hao kweli ndio Waumini}.

Jibu ni kwamba ninaapa kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu mimi sijui kama na Mimi ni miongoni mwao au sio miongoni mwao!

Na imani ya kweli humrithisha mwenye kuimiliki, Usalama na Amani pamoja na maisha mazuri ambayo hayapatikani isipokuwa kwa imani hiyo.

Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

بسم الله الرحمن الرحيم.

{مَنْ عَمِلَ صَالِحًا مِنْ ذَكَرٍ أَوْ أُنْثَى وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَنُحْيِيَنَّهُ حَيَاةً طَيِّبَةً}

{Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini, tutamhuisha maisha mema;...}.

Na anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

بسم الله الرحمن الرحيم.

{الَّذِينَ آمَنُوا وَتَطْمَئِنُّ قُلُوبُهُمْ بِذِكْرِ اللَّهِ أَلَا بِذِكْرِ اللَّهِ تَطْمَئِنُّ الْقُلُوبُ}

{Wale walio amini na zikatua nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua!}

Na ninaisema kauli yangu hii, na ninamwomba msamaha Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili yenu na kwa ajili yangu.

**(٢)**

AL-HAMDULILLAHI WA ASSALATU WA ASSALAMU ALA SAYYEDNA MUHAMMAD WA ALA AALIHI WA SAHBIHI AJMAEEN.

Hotuba yetu ya pili ni juu ya mwezi wa Ramadhani ni mwazi wa kuwajenga wanaume.

*　　*　　*

**Sifa zote njema ni zake mwenyezi Mungu Mtukufu Mlezi wa viumbe vyote. Na ninashuhudia kwamba hakuna yoyote anayestahili kuabudiwa kwa Haki isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, yeye pekee asiye na mshirika wake, na ninashuhudia kwamba Bwana wetu Muhammad ni Mja na ni Mtume wake, na rehma na amani ziwe juu ya Mtume wa Mwisho katika Mitume, na Manabii wake**

**Mwenyezi Mungu Mtukufu, Bwana wetu Muhammad S.A.W, na Jamaa zake, na Maswahaba wake wote, na atakayewafuata kwa Wema mpaka siku ya Malipo.**

Ndugu zangu Waislamu.

Ukiwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ni Mwezi wa Imani, huu ni mwezi wa kuwajenga Watu pia. Kwani Swaumu yake ni Chuo cha kivitendo kinachowadhihirisha Wanaume wa shoka. Anasema Ahmad Shaukiy: Swaumu ni kunyimwa kisheria, na kufunzwa kwa njaa, na kumnyenyekea Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa unyenyekevu, na kila Faradhi ina Hekima yake na Hekima hii uwazi wake ni adhabu na undani wake ni rehma, huleta ishara ya Kuhurumia, na huchochea ukweli, huvunja kiburi na hufundisha uvumilivu na huzoesha Wema, mpaka mtu anapokuwa na njaa kwa shibe elfu moja, na humharamishia mbadhirifu sababu za kustarehe, mwenye kunyimwa huko anajua jinsi kunavyotokea na jinsi kunavyomuua pindi anapokosea.

Hakika kwa mwenye kuzingatia katika Qurani Tukufu ataona kwamba ushujaa ni Sifa ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu hakumpa isipokuwa yule mwenye kumiliki nyenzo zake, ambazo miongoni mwake ni: Ahadi ya kweli na Mwenyezi Mungu Mtukufu, bila ya kubadilisha au kubadilika, au kukengeuka.

Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

بسم الله الرحمن الرحيم. {مِنَ الْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ عَلَيْهِ فَمِنْهُمْ مَنْ قَضَى نَحْبَهُ وَمِنْهُمْ مَنْ يَنْتَظِرُ وَمَا بَدَّلُوا تَبْدِيلا}

{Miongoni mwa Waumini wapo watu walio timiza waliyo ahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwisha kufa, na baadhi wanangojea, wala hawakubadilisha (ahadi) hata kidogo}.

Kama ambavyo, Wanaume wa shoka ni wale walioziuza nafsi zao na mali zao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mola wa Walimwengu wote. Na haya

yanadhihirika katika kujitoa muhanga kwa Nafsi na Mali kwa ajili ya njia ya Dini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, au Nchi, au Heshima, kwa kuzitafuta radhi zake Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

بسم الله الرحمن الرحيم.{إِنَّ اللَّهَ اشْتَرَى مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنْفُسَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ بِأَنَّ لَهُمُ الْجَنَّةَ يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيَقْتُلُونَ وَيُقْتَلُونَ وَعْدًا عَلَيْهِ حَقًّا فِي التَّوْرَاةِ وَالإِنْجِيلِ وَالْقُرْآنِ وَمَنْ أَوْفَى بِعَهْدِهِ مِنَ اللَّهِ فَاسْتَبْشِرُوا بِبَيْعِكُمُ الَّذِي بَايَعْتُمْ بِهِ وَذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ}.

{Hakika Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waumini nafsi zao na mali zao kwa kuwa wao watapata Pepo. Wanapigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu - wanauwa na wanauwawa. Hii ni ahadi aliyo jilazimisha kwa Haki katika Taurati na Injili na Qur'ani. Na nani atimizae ahadi kuliko Mwenyezi Mungu? Basi furahini kwa biashara yenu mliyo fanya naye. Na huko ndiko kufuzu kukubwa}.

Hakika ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ni mwezi wa kuiimarisha Misikiti kwa kuswali nyakati za usiku, nazo ni miongoni mwa vitendea kazi muhimu vya kujengea Utu na kuwatengeneza Wanaume wa kweli.Kwa hivyo

Mwenyezi Mungu Mtukufu alimweleza Mtume wake S.A.W:

**بسم الله الرحمن الرحيم**

{يَا أَيُّهَا الْمُزَّمِّلُ * قُمِ اللَّيْلَ إِلَّا قَلِيلًا * نِصْفَهُ أَوِ انْقُصْ مِنْهُ قَلِيلًا * أَوْ زِدْ عَلَيْهِ وَرَتِّلِ الْقُرْآنَ تَرْتِيلًا* إِنَّا سَنُلْقِي عَلَيْكَ قَوْلًا ثَقِيلًا * إِنَّ نَاشِئَةَ اللَّيْلِ هِيَ أَشَدُّ وَطْئًا وَأَقْوَمُ قِيلًا}

{Ewe uliye jifunika! Kesha usiku kucha, ila kidogo tu! Nusu yake, au ipunguze kidogo. Au izidishe - na soma Qur'ani kwa utaratibu na utungo. Hakika Sisi

tutakuteremshia kauli nzito. Hakika kuamka usiku kunawafikiana zaidi na moyo, na maneno yake yanatua zaidi}.

Pia Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

بسم الله الرحمن الرحيم.

{فِي بُيُوتٍ أَذِنَ اللَّهُ أَنْ تُرْفَعَ وَيُذْكَرَ فِيهَا اسْمُهُ يُسَبِّحُ لَهُ فِيهَا بِالْغُدُوِّ وَالْآصَالِ رِجَالٌ لَا تُلْهِيهِمْ تِجَارَةٌ وَلَا بَيْعٌ عَنْ ذِكْرِ اللَّهِ ***وَإِقَامِ الصَّلَاةِ وَإِيتَاءِ الزَّكَاةِ يَخَافُونَ يَوْمًا تَتَقَلَّبُ فِيهِ الْقُلُوبُ وَالْأَبْصَارُ}

{Katika Nyumba ambazo Mwenyezi Mungu ameamrisha zitukuzwe, na humo litajwe jina lake, wanamtakasa humo asubuhi na jioni.Watu ambao biashara wala , na kushika Sala, kuuza hakuwashughulishi na kumdhukuru Mwenyezi Mungu**** na kutoa Zaka. Wanaikhofu Siku ambayo nyoyo na macho yatageuka}.

Na anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

بسم الله الرحمن الرحيم. {كَانُوا قَلِيلًا مِنَ اللَّيْلِ مَا يَهْجَعُونَ* وَبِالْأَسْحَارِ هُمْ يَسْتَغْفِرُونَ}

{Walikuwa wakilala kidogo tu usiku.Na kabla ya alfajiri wakiomba maghfira}.

**Na anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:**

**بسم الله الرحمن الرحيم.{تَتَجَافَى جُنُوبُهُمْ عَنِ الْمَضَاجِعِ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ خَوْفًا وَطَمَعًا وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنْفِقُونَ*فَلَا تَعْلَمُ نَفْسٌ مَا أُخْفِيَ لَهُمْ مِنْ قُرَّةِ أَعْيُنٍ جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ}.**

{Mbavu zao zinaachana na vitanda kwa kumwomba Mola wao Mlezi kwa khofu na kutumaini, na hutoa kutokana na tulivyo waruzuku.Nafsi yoyote haijui waliyo fichiwa katika hayo yanayo furahisha macho - ni malipo ya yale waliyo kuwa wakiyatenda}.

Hakika Swala za Usiku ni katika mambo tunayopaswa kuyapupia, na hasa katika kumi la mwisho la mwezi mtukufu wa Ramadhani, tukimwiga Mtume S.A.W. Mtume S.A.W alikuwa anajitahidi sana katika masiku ya kumi hili la mwisho kuliko masiku mengine.

Kutoka kwa Aisha R.A, amesema: Mtume S.A.W alikuwa linapoingia kumi la mwisho hujitahidi kwa ibada kadri ya uwezo wake, kuuhuisha usiku kwa Ibada, na alikuwa akiwaamsha Watu wake. Na amesema pia Bi Aisha R.A: Mtume S.A.W alikuwa akichanganya siku ishirini kwa Swala na kulala, na alipofika kumi la mwisho aliongeza zaidi ibada na kufanya juhudi kubwa zaidi. Na katika mapokezi mengine amesema Bi Aisha: Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu alikuwa anajitahidi zaidi katika kumi la mwisho la mwezi wa Ramadhani kwa Ibada ambazo alikuwa hafanyi hivyo katika masiku mengine.

Hakika mwezi mtukufu wa Ramadhani huwajenga wanaume kwa kuzuia matamanio ya Nafsi zao, na kwa utulivu, na kwa Mzinduko wa dhamira zao, na kwa kuidhibiti mienendo yao, na ubora wa kuchukua hatua, na kuiyaweka juu maadili ya maumbile ya kibinadamu na Tabia njema zinazo ipangilia mienendo ya mwanadamu na kumfanya anyooke katika kila jambo la maisha yake, akazilinda Haki na kutekeleza majukumu yake ipasavyo, na akawa anahangaikia kuleta kila aina ya heri na wema kwake, kwa jamii yake, kwa nchi yake na kwa umma wake, na kwa hivyo haya yote yanaonekana kwa kuleta utulivu wa Jamii na maendeleo yake, na kuenea kwa moyo wa Upendo na Mjongeleano wa dhati na kuhurumiana, pamoja na mengi mengine miongoni mwa Maana nzuri ambazo zinachangia maendeleo ya watu na kustaarabika kwao.

Kwa hiyo tupupie katika kuyatumia masiku haya kwa kumtaja Mwenyezi Mungu Mtukufu na kwa Dua, na kuisoma Qurani Tukufu, na kujitahidi katika kufanya kila jambo linaloweza kutukurubisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, mpaka tusiwe katika walionyimwa rehma zake Mwenyezi Mungu Mtukufu katika masiku haya yaliyobarikiwa, ambapo anasema Mtume wetu S.A.W: Hakika ana Mola wenu katika masiku ya uhai wenu tunu. Basi kuweni karibu nazo: huwenda mmoja wenu akapatwa na moja kati ya tunu hizo, akawa si mwenye kuwa mwovu baadaye milele.

**Mola wetu tukubalie sisi hakika Wewe ni Msikivu na ni Mjuzi, na utukubalie toba zetu kwani hakika Wewe ni mwingi wa Kukubali toba na ni mwingi wa Kurehemu na Dua yetu ya mwisho ni Alhamdulillahi Rabi Alaalameen.**